TANGAZO LA SERIKALI NA.140 la tarehe 3/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA MALOPOKELO NA OLD TANDAHIMBA YA MWAKA 2023.

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Malopokelo na Old Tandahimba ya Mwaka 2023.

Kutangaza Eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Kuandaa na kuhifadhi Mipango ya jumla na kina

3. Mipango ya jumla na kina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.

———

JEDWALI

———

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MT1 yenye majira - nukta 568737SM , 8811568KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa $00^0$ 06'29'' kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MT2 yenye majira - nukta 568740MS ,8811896KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa $61^0$ 47'12''kwa umbali wa kilomita 2.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MT3 yenye majira - nukta 566544MS, 8810720KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki hadi barabara ya Newala - Mtwara katika uelekeo wa $79^0$ 56'26'' kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MT4 yenye majira - nukta 566871MS, 8810329KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $80^0$ 09'39'' kwa umbali wa kilomita 0.465 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MT5 yenye majira - nukta 567331MS, 8810253KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Mashariki katika uelekeo wa $69^0$ 12'59''kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MT6 yenye majira - nukta 567616MS, 8809418KZ ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $02^0$ 07'44'' kwa umbali wa kilomita 0.9 kwenye hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MT7 yenye majira - nukta 568140MS, 8809230KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa $73^0$ 37'08'' kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MT8 yenye majira –nukta 568174MS, 8810137KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Masharki katika uelekeo wa $02^0$ 06'55'' kwa umbali wa kilomita 1.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MT9 yenye majira -nukta 568787MS, 8810318KZ, baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa $02^0$ 06'55'kwa umbali wa kilomita 1.238 hadi ulipoanzia."

| | |
|---|---|
| Dodoma | ANGELINE S. MABULA |
| 6 Februari, 2023 | *Waziri wa Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi* |